TANGAZO LA SERIKALI NA. 183 la tarehe 21/3/2025

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 284)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA USAFIRI MAJINI ZA UBEBAJI WA SHEHENA NA MIZIGO YABISI NA FUELI ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 381 la 2024

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usafiri Majini za Ubebaji wa Shehena ya Mizigo Yabisi na Fueli za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usafiri Majini za Ubebaji wa Shehena ya Mizigo Yabisi na Fueli za Mwaka 2024, ambazo hapa zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri za misamiati mipya ifuatayo kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti kama ifuatavyo:

""shehena ya mizigo oevu" maana yake ni kiasi kikubwa cha bidhaa za kimiminika zinazosafirishwa kwa wingi isiyofungashwa kwenye makasha binafsi na inajumuisha vimiminika mbalimbali kama vile mafuta ghafi, bidhaa za petroli, kemikali, gesi miminika au chakula cha kiwango cha kimiminika;

"meli za roro" maana yake ni meli za mizigo zilizoundwa kubeba mizigo kama vile magari, pikipiki, malori, mabasi, trela, na magari ya reli ambayo huendeshwa na kutoka nje ya meli kwa magurudumu yao yenyewe au kutumia gari la jukwaa kama vile kisafirishaji kinachojiendesha chenyewe;".

Dodoma
5 Machi, 2025

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Uchukuzi*